

ASb
approved




Siku za wiki
Ubongo
Ubongo

Kiswahili




Kila wiki ina siku saba:

Jumatatu,
Jumanne,
Jumatano,
Alhamisi, Ijumaa,
Jumamosi na
Jumapili.



Siku ninayoipenda
ni Jumatatu. Ni siku
ya kwanza ya wiki.

Huwa ninaenda
shule siku ya
Jumatatu.




Jumanne ni siku ya
pili ya wiki.

Inafuata baada ya
Jumatatu.



Jumanne huwa
tunacheza michezo
tunayoipenda
shuleni.



Jumatano ni siku ya tatu ya wiki.

Iko katikati ya wiki.



Siku ya Jumatano
huwa tunapaka
rangi shuleni.



Baada ya
Jumatano inafuata
Alhamisi.

Alhamisi ni siku ya
nne ya wiki.



Watoto wakubwa
hutusimulia hadithi
siku ya Alhamisi.



Ijumaa ni siku ya tano ya wiki.

Ijumaa ni siku ya mwisho ya wiki kwenda shule.



Tunapenda kula
sambusa siku ya
Ijumaa.



Mchana, tukifika
nyumbani huwa
tunajitayarisha
kwa wikiendi
kuanza.



Jumamosi ni siku
ya sita ya wiki.



Siku ya Jumamosi
huwa tunaangalia
katuni...



...na kwenda
sokoni.



Jumamosi na
Jumapili ni siku za
kucheza na
kupumzika.



Jumamosi huwa
tunaenda sokoni
kununua matunda
ninayoyapenda
sana.



Jumapili ni siku ya mwisho ya wiki. Ni siku ya mapumziko kabla ya kuanza wiki mpya.

Jioni huwa ninaandaa vifaa vyangu vya shule.



Wiki ina siku saba:

Jumatatu,
Jumanne,
Jumatano,
Alhamisi, Ijumaa,
Jumamosi na
Jumapili.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Siku za wiki

Author - Ubongo

Illustration - Ubongo

Language - Kiswahili

Level - First sentences

© African Storybook Initiative 2021

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source Akili and Me by Ubongo

